# MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI

## TAARIFA KWA UMMA

| | | |
|---|---|---|
| Tarehe | : | **28 Februari, 2025** |
| **Somo** | : | **TAARIFA YA MATOKEO YA MITIHANI YA TAIFA YA UFUNDI STADI KWA MSIMU WA DESEMBA 2024** |

---

### 1.0 UTANGULIZI

Katika kipindi cha Mitihani ya mwezi Desemba 2024 jumla ya watahiniwa 41,331 walijitokeza kufanya Mitihani ya Taifa ya Ufundi Stadi katika Programu za **CBA** yaani Mitihani ya Taifa ya Ufundi Stadi ya Kupima Umahiri kwa Ngazi ya 1, 2 na ya 3, **NABE** yaani Mitihani ya Taaluma ya Biashara, Uanagenzi Pacha (Dual Apprenticeship) na Programu rasmi ya Uanagenzi kwa fani za madini (IMTT).

### 2.0 MATOKEO YA MITIHANI YA UFUNDI STADI KATIKA MFUMO WA CBA (COMPETENCE BASED ASSESSMENT).

Katika Mitihani ya Ufundi Stadi iliyofanyika mwezi Desemba, 2024, jumla ya wanafunzi 40,666 walifanikiwa kufanya Mitihani ya Taifa ya Ufundi Stadi kwa mfumo wa CBA, ambapo kiwango cha ufaulu kwa Programu hiyo ni asilimia 86.1. Mchanganuo wa ufaulu kwa kila ngazi ni kama ifuatavyo:

#### 2.1. Matokeo ya Mitihani ya Ufundi Stadi Ngazi ya Kwanza (Level 1)

Mitihani ya Ufundi Stadi kwa mfumo wa CBA ilitahini jumla ya wanafunzi16,446 na matokeo ya Mitihani katika Ngazi hii yameonesha kuwa jumla ya wanafunzi 14,036 (85.3%) walifaulu Mitihani ya Ufundi Stadi ambapo kati yao, wa kiume walikuwa 9,118 (83.4%) na wakike ni 4,918 (89.2%).

#### 2.2. Matokeo ya Mitihani ya Ufundi Stadi Ngazi ya Pili (Level 2)

Mitihani ya Ufundi Stadi kwa mfumo wa CBA ilitahini jumla ya wanafunzi 21,676 na matokeo ya Mitihani katika ngazi hii yameonesha kuwa jumla ya wanafunzi 18,964 (87.5%) walifaulu Mitihani ya Ufundi Stadi ambapo kati yao, wakiume walikuwa 12,732 (87.0%) na wakike ni 6,232 (88.5%).

#### 2.3. Matokeo ya Mitihani ya Ufundi Stadi Ngazi ya Tatu (Level 3)

Mitihani ya Ufundi Stadi kwa mfumo wa CBA ilitahini jumla ya wanafunzi 2,544 na matokeo ya Mitihani katika ngazi hii yameonesha kuwa jumla ya wanafunzi

1,999 sawa na asilimia 78.6% walifaulu Mitihani ya Ufundi Stadi ambapo kati yao wakiume ni 923 (74.9%) na wakike ni1, 076 (82.1%).

Watahiniwa 5,667 (13.9%) kati ya 40,666 waliofanya Mitihani ya CBA kwa Ngazi ya 1, 2 na ya 3 wanapaswa kurudia Mitihani hiyo.

## 3.0 MATOKEO YA MITIHANI YA TAALUMA YA BIASHARA - NABE (NATIONAL BUSINESS EXAMINATIONS)

Katika Mitihani ya Taaluma ya Biashara iliyofanyika Desemba, 2024 jumla ya wanafunzi 283 walijitokeza kufanya Mitihani katika hatua ya 1, 2 na 3 (Stage I, 2 and 3). Jumla ya wanafunzi 65 (23.0%) walifaulu Mitihani hiyo kati yao, wakiume ni 17 (56.7%) na wakike ni 48 (19.0%). Wanafunzi 218 (77.0 %) wanapaswa kurudia Mitihani hiyo.

## 4.0 PROGRAMU YA UANAGENZI PACHA (DUAL APPRENTICESHIP TRAINING SYSTEM)

Programu hii ya kutambua na kukuza ujuzi wa Wanagenzi inaendeshwa kwa Mfumo shirikishi wa mafunzo baina ya vyuo vya Ufundi na Viwanda. Jumla ya Wanagenzi Pacha (Dual) 230 (75.2%) kati ya Wanagenzi 306 wamefaulu.

## 5.0 PROGRAMU RASMI YA UANAGENZI KWA FANI ZA MADINI (INTERGRATED MINING TECHNICAL TRAINING - IMTT)

Programu hii ya kutambua na kukuza ujuzi wa Wanagenzi inaendeshwa kwa Mfumo shirikishi wa mafunzo baina ya Vyuo vya Ufundi Stadi na Sekta ya madini. Jumla ya Wanagenzi 61 (80.3%) kati ya Wanagenzi 76 wamefaulu.

## 6.0 WATAHINIWA WALIOFUTIWA MATOKEO



Watahiniwa wawili (0.01%) waliojihusisha na vitendo vya udanganyifu katika kipindi cha kufanya Mitihani ya mwezi Desemba 2024 wamefutiwa matokeo yao baada ya kuwasilishwa kwa vithibitisho.

**IMETOLEWA NA**
**MKURUGENZI MKUU**
**MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI**




CPA. Anthony M. Kasore
**MKURUGENZI MKUU**

## Vyuo Vilivyosajiliwa Kufanya Mitihani Kwa Msimu Wa Desemba, 2024

| IDADI YA VYUO | ASILIMIA |
| --- | --- |
|  |  |

# MUHTASARI WA MATOKEO – MSIMU WA DESEMBA 2024




| | CBA | NABE | IMTT | DAT |
|---|---|---|---|---|
| Idadi ya watahiniwa | 40666 | 283 | 76 | 306 |
| Ufaulu (%) | 86.1 | 23 | 80.3 | 75.2 |

Idadi ya watahiniwa    Ufaulu (%)